# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE.

**NAMBA YA KITUO: S.8456**
SHULE YA SEKONDARI MLOGOLO
S.L.P 139,
**SIKONGE-TABORA.**
TAREHE………………..

**NAMBA ZA SIMU:**
MKUU WA SHULE: 0684125528/0769365433
MAKAMU MKUU WA SHULE:
PATRON: 0681992561
MATRON: 0783432853

**Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi,**
……………………………………
S.L.P…………………………
……………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026**

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2025/2026 mkondo wa ……………….. ……………………. Shule hii ina mchepuo wa **Ufundi/Amali Uhandisi.** Shule ina mchanganyiko wa wasichana na wavulana kwa kidato cha Kwanza hadi cha Nne. Shule ya sekondari Mlogolo ipo umbali wa kilomita sita (06km) kaskazini mwa makao makuu ya wilaya ya Sikonge karibu na shule ya msingi Mlogolo barabara iendayo Tabora/ Mpanda.
Usafiri wa pikipiki /bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi Sikonge na nauli kwa pikipiki 2000/=, na bajaji 4000/= .
Muhula wa kwanza masomo unaanza tarehe …/…/2026 Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe …./…/2026. na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe…./…/2026

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**
**2.1. Sare ya shule**

**2.1.1 WASICHANA**

a. Sketi mbili rangi ya Aqua green mshono wa linda box pana, urefu wa sketi ufike kwenye kifundo cha mguu [kitambaa kizito] na wanafunzi wa kiislamu ; nusu kanzu nyeupe mbili kitambaa cha tetroni nzito na hijabu/juba nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua na zisizo na urembo wa aina yoyote.
b. Shati nyeupe mikono mifupi Jozi mbili **(2)**
c. Ovaroli 01 ya rangi ya "**Dark blue**"
d. Shuka Rangi ya Pinki Jozi mbili (2),
e. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, siyo buti na visiwe na visigino virefu Jozi mbili (2),
f. Soksi rangi nyeupe jozi mbili,(2)

g. Shamba dress/gauni mbili za rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya kushindia urefu ni mpaka kwenye kifundo cha mguu na mshono wa gauni ni solo.kwa wale wanaovaa hijabu /juba zifanane na rangi ya gauni

h. Khanga Kipande kimoja na kitenge kipande kimoja.

i. Sweta la rangi ya Maroon.

j. Tai mbili za rangi ya Aqua green.

k. T-sheti moja ya rangi ya dark blue, zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 15,000/=

l. **Vifaa vya michezo**: Raba au viatu vyeupe vya michezo, Jezi na Bukta zote ziwe **na rangi ya light blue** na **"Track Suit" ya rangi ya light blue** yenye mstari mweupe.

**NB: Hairuhusiwi mwanafunzi kuvaa sketi fupi, zinazobana, zisizo na marinda, zenye mpasuo na zilizoshonwa kwa Kitambaa angavu (Transparent).**

**2.1.2 WAVULANA:**

a. Suruali mbili (2) Rangi ya Aqua green.
b. Shati Nyeupe mikono mifupi jozi mbili (2)
c. Ovaroli 01 ya rangi ya **"Dark blue"**
d. Shuka Rangi ya bluu bahari Jozi mbili (2),
e. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba, siyo buti na visiwe na visigino virefu Jozi mbili (2),
f. Soksi rangi nyeusi Jozi mbili (2),
g. Tai mbili za rangi ya Aqua green.
h. Mkanda mweusi wenye kifungio cha kawaida.
i. Nguo za kushindia- **Suruali rangi nyeusi jozi mbili na fulana rangi ya dark blue zenye kola (maarufu kama "form six") zenye Nembo ya Shule** na zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 15,000
j. **Vifaa vya michezo**: Raba au viatu vyovyote vya michezo, Jezi na Bukta zote ziwe **na rangi ya light blue na "Track Suit" ya rangi ya light blue**

**NB: Hairuhusiwi mwanafunzi kuvaa suruali zinazobana (vimodo), vikoti, makoti, vilemba, kofia, vizibao kama sehemu ya sare ya shule.**
***Suruali chini ziwe na upana wa inchi 17 au 18, mbele iwe na rinda mbili ("Celebration") kila upande na mifuko miwili ya "cross", na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kuwekea mkanda.**

**2.2. Mahitaji mengine MUHIMU ambayo mwanafunzi anatakiwa aje nayo shuleni.**
**2.2.1. Mwanafunzi ajapo shuleni aje na :-**

i. Madaftari ya kutosha Counter books Quire 3 [Idadi ni 12], penseli, kalamu, mathematical set(compass) na rula.
ii. Godoro futi 2.5x 6
iii. Mashuka pea mbili rangi ya pink /bluu bahari,blanketi moja , mto wa kulalia, foronya moja na Chandarua cha duara chenye rangi nyeupe.
iv. Sanduku la bati (trunker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake
v. Taulo moja (1) kwa matumizi binafsi
vi. Vyombo vya chakula.
vii. Tochi ndogo ya betri au solar kwa matumizi ya dharura umeme unapokatika.
viii. Ndoo mbili ndogo zenye mfuniko na dumu moja la lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa

ix. Karatasi nyeupe rimu 2 kwa mwaka.
x. Aje na vifaa vya usafi vifuatavyo :- ufagio wa ndani{soft broom 1} na ufagio wa nje (chelewa 1 yenye mpini mrefu na imara), jembe lenye mpini 1, kwanja 1na reki 1.
xi. Fedha kama vile nauli ya kurudia nyumbani/Fedha za matumizi madogo madogo nk. Mwanafunzi aweke Fedha za ziada kwenye Akaunti yake Benki au ziwekwe Ofisi ya *fedha ya shule ambapo, Mwanafunzi atasaini kila anapochukua fedha.*
xii. Picha 4 **(Pass Port size)** zipigwe na sare ya shule, pia huduma hii inaweza kupatikana karibu na shule kwa gharama ya Tshs. 3,000/=

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo :-

i. Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi na jamii yote kwa ujumla .
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli zifanyikazo shuleni.
iii. Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.
iv. Kufahamu na kuheshimu mipaka ya shule.
v. Kutotoka nje ya shule bila sare ya shule na ruhusa ya maandishi.
vi. Kutunza usafi binafsi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
*vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni.*
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Ni marufuku kuwa bwenini wakati wa
ix. shughuli za darasani.
x. Kuheshimu na kusimama wima bendera ya Taifa inapopandishwa au kushushwa na wimbo wa Taifa unapoimbwa.
xi. Kuishi maisha ya ushirikiano na upendo na wenzako pamoja na jumuiya yote ya shule
xii. Kutotoa lugha ya matusi, kuzomea au kuanzisha fujo na kuanzisha au kushiriki katika migomo.
xiii. Kusalimia wafanyakazi au mtu yeyote anayestahili anapopita ndani au nje ya darasa,
xiv. Kutomiliki kifaa chochote cha umeme kama vile pasi,chaja na simu.
xv. Kulipa michango yote ya shule kwa wakati ili kuepuka usumbufu.
xvi. Kufanya mitihani yote ya shule.
xvii. Kuvaa kitambulisho cha shule wakati wote ndani na nje ya shule.

**MUHIMU:**

1. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
3. Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani kwani atashindia sare za kushindia zilizoainishwa.
4. Mwanafunzi anaporipoti aje na fomu hii ikiwa na karatasi zote
5. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, kaka na dada na si mtu mwingine. Taarifa za msiba ziletwe moja kwa moja kwa mkuu wa shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.
6. Wageni wanaotambulika shuleni ni wale tu walioandikishwa kwenye faili la wanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula, mara mbili [2] kwa mwaka (kukiwa na ulazima wa kufanya hivyo.)
7. Likizo zote kwa mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwao.
8. Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia shuleni zaidi ya saa 12 jioni isipokuwa kwa dharura na *taarifa kwa uongozi wa shule.*

## 4.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZA KUFUKUZWA SHULE

1.Wizi.
2.Uasherati, ushoga na Ubakaji.
3.Ulevi wa aina zote na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kuberi na kadhalika.
4.Kupigana au kupiga.
5.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, binafsi au ya mwenzako.
6.Kudharau Bendera ya Taifa.
7.Kuwa mjamzito/kupata mimba/kutoa mimba
8.Kuoa au kuolewa.
9.Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
10.Kufanya jaribio lolote la kujiua.
11.Kukataa adhabu kwa makusudi
12.Kuwa na simu/laini ya simu ya mkononi shuleni.
13.Kutembelea majumba ya starehe na ya kulala wageni.
14.Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.

## 5.MAENEO YA KUFANYA KAZI

### A. MABWENINI

5.1 Kila mwanafunzi atapangiwa na mwalimu wa bweni eneo la kufanya kazi asubuhi na jioni *baada ya saa za darasani.*

5.2 Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayeacha kuhudumia eneo lake kikamilifu. Aidha kila asubuhi/jioni mwanafunzi anatakiwa kufanya usafi katika bweni, choo, bwalo, eneo nk. Kama atakavyopangiwa na mwalimu/viongozi wake.

5.3 Ni **marufuku** kuwa bwenini wakati ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani/miradi/michezo/Roll-check/Baraza nk.

**B. DARASANI**

1. Wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani muda wote wa vipindi.
2. Darasa liwe safi (**lisiwe na buibui, vumbi, karatasi** nk) Mwalimu wa Darasa atakagua vyumba vya madarasa mara kwa mara. Kiongozi wa darasa na kiranja wahakikishe kila darasa ni safi. Orodha ya zamu na usafi itapangwa na Kiranja.
3 Wakati mwanafunzi akiwa darasani anatakiwa afanye yafuatayo:-
(i) Mwanafunzi asipige kelele/asitoketoke darasani
(ii) Mwanafunzi aulize na kujibu maswali
*(iii) Mwanafunzi afanye test/mazoezi/majaribio yote kwa uwezo wake wote. Kila* mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/test kwa kila somo.
(iv) Viti/madawati yapangwe kwenye mistari iliyonyooka
(v) Mwanafunzi **analazimika** kuhudhuria vipindi vyote kwa siku.
(vi) **"Private Study"** iliyopo kwenye ratiba ya siku hiyo ni **lazima** ifanyike darasani na sio nje ya darasa au mahali pengine.
(vii) Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati/taa/switch n.k. kutoka darasa moja kwenda mahali pengine. Viongozi wa wanafunzi (**monita na viranja**) wahakikishe kwamba hakuna kifaa kilichohamishwa kutoka darasa moja kwenda mahali pengine bila kibali cha mwalimu wa darasa.
(viii) Ni marufuku kuunganisha umeme katika jengo lolote la shule bila kibali cha uongozi wa shule. Aidha, matumizi ya pasi na **"heaters"** bwenini hayakubaliki/hayaruhusiwi.

**6. CHAKULA**

1. Shule inaandaa Chakula kwa ajili ya Wanafunzi wote kila Siku. Kila Mwanafunzi **ni lazima** ale chakula hicho kinachoandaliwa na shule. Chakula kiliwe ndani ya Bwalo, na ni marufuku kupeleka chakula Bwenini au mahali pengine popote nje ya Bwalo bila **KIBALI** maalum. **Aidha,**
**2. Hakuna Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule kwa ajili ya kutafuta Chakula.**

**7. UTAMADUNI NA MICHEZO**

1.Shule ina michezo mbalimbali kila mwanafunzi ni **LAZIMA** ashiriki kikamilifu katika michezo angalau mchezo mmoja au zaidi. Utaratibu umeandaliwa na Mratibu wa michezo na Mwalimu Mwandamizi Malezi & Utamaduni.
2. Mwanafunzi ambaye hawezi kushiriki katika michezo hiyo awe na barua ya daktari na apewe kibali na Mkuu wa Shule.
3. Mashindano yatafanyika kila muhula na zawadi zitatolewa kwa washindi kulingana na Bajeti ya Shule.

**8. HUDUMA MUHIMU**
**MATIBABU:**

1.Shule haina Zahanati kila mwanafunzi mwenye tatizo la afya yake aingiapo shuleni atoe taarifa.
2.Mwanafunzi haruhusiwi kuweka dawa bwenini. Dawa zote zikabidhiwe ambapo mwanafunzi atapewa dawa kwa kiasi/kiwango kinachojulikana na mtaalamu.
3. Aidha, **kila Mwanafunzi, anatakiwa awe na Kadi ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), ili kupanua Wigo wa Huduma za Afya katika Hospitali . (Gharama za Matibabu , zitagharamiwa na Mzazi/Mlezi) Gharama za (NHIF) ni 50,400/= kwa Hospitali zote zinazotumia Bima ya Afya.**
4. Mwanafunzi atakayezidiwa mzazi/mlezi ataarifiwa.

***9. KURUDI SHULENI BAADA YA LIKIZO***

Ni jukumu la mzazi kuona kwamba mwanao anarudi shuleni siku moja kabla ya siku ya kufunguliwa shule. Shule ikishirikiana na Bodi ya shule wana mikakati ya kuimarisha taaluma ambapo mwanafunzi atatakiwa kuripoti shuleni kwa muda uliopangwa kuepuka kuchelewa masomo.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- Mkuu wa shule: 0684125528/0769365433
- Mwandamizi Malezi: 0681992561/0783432853

*Karibu sana katika shule hii.*

.......................

**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MLOGOLO
S.L.P 139-SIKONGE

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MLOGOLO SECONDARY SCHOOL**
**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I Entrants.
Pupil's full name............................................................................
Age/Years ..........................................Sex..........................................
Blood found (red and white)..................................................................
Stool examination.....................................................................
Urinalysis..............................................................................
Venereal Diseases test..................................................................
T.B. Test: ..............................................................................
Eye Test.... ......................................................'.................................
Ears..........................................................................................
Chest.........................................................................................
Spleen.......................................................................................
Abdomen.......................................................................
Urine for Pregnant.......................................................................
ADDITIONAL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. Infections, chronic or family disease.
..............................................................................................................
..............................................................................................................
..............................................................................................................
..........................

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.
Signature: ..................................
Station..................................................Date:.......................
Official stamp.........................................

*FOMU NA.2*

**SHULE YA SEKONDARI MLOGOLO**
**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1.JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………

2.KABILA…………………………………

3.TAREHE Y A KUZALIWA ... . . ... .....MWEZI.... ......... MWAKA..................

4.AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA ..................................................

5.MKOA WA………………………………………………..

6.DINI…………………………………………………DHEHEBU………………………

7.JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………..

(Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)

8. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…………………….........(KIJIJI)

………………………………..(TARAFA)

………………………………………(WILAYA)

…………………………………………..(MKOA)

Na.za simu 1…………………………………

2…………………………………………..

9. KAZI YA BABA/MLEZI…………………………………………………………………

10. KAZI YA MAMA……………………............... ………………………………......

11.Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari)

12.Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (majina matatu), anuani zao kamili na namba zao za simu

a. Ndugu..... ……………………………………………….....Uhusiano………………..
simu…………………………………..

b. Ndugu..... …………………………………………………......Uhusiano………………
simu…………………………………..

c. Ndugu..... ……………………………………………………...Uhusiano………………
simu………………………………………

**SAINI YA MWANAFUNZI** …………………… **SAINI YAMZAZI/MLEZI**……………

## MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi....... ..............................................................(Jina kamili) ambaye ni mwanafunzi nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahala pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

**Saini ya mwanafunzi....................................**
**Tarehe.............................**
**Shahidi**
**Jina kamili...................................................**
**Saini.........................**
**Tarehe.........................**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi........ ........................................................................(Jina kamili) ambaye ni mzazi /mlezi wa.......... ..............................................................Kidato cha .....................nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii na naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.

Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

**Saini ya Mzazi/Mlezi.................................**

**Anunani kamili.......................................**

**Tarehe.............................**

**Simu..........................**